

Jaza pengo kwa kuchagua jibu bora zaidi.

Siku _____ 1 _____ nilifika _____ 2 _____ nikiwa nimechoka _____ 3 _____ Nilikuwa
nikitoka _____ 4 _____ mwilini, nilielekea _____ 5 _____ na kuoga, _____ 6 _____ maji yaliyokuwa
_____ 7 _____ Baada _____ 8 _____ hayo nilienda _____ 9 _____
palipokuwa pameandaliwa _____ 10 _____ mtamu sana.

A

1. mmoja
2. mji
3. zana
4. chasho
5. bafuni
6. na
7. kali
8. ya
9. huko
10. mno

B

1. moja
2. nyumba
3. kidogo
4. jacho
5. bafu
6. kwa
7. baridi
8. la
9. pale
10. mro

C

1. kimoja
2. nyumbani
3. mwisho
4. vumbi
5. uwanjani
6. ni
7. ghali
8. cha
9. mle
10. mloo

D

1. limoja
2. shamba
3. sana
4. jasho
5. shuleni
6. pia
7. chini
8. kwa
9. kwa
10. mlo

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.

Ngamia ni mnyama wa ajabu sana. Anashingo ndefu, miguu mirefu na nundu mgongoni. Watu wanaoishi jangwani humtumia ngamia kwa njia mbalimbali. Ngamia anaweza kwenda mwendo mrefu bila ya kuchoka. Akinywa maji, anaweza kukaa kwa muda mrefu bila ya kuhitaji maji. Kwato zake zimeumbwa kwa njia inayomwezesha kutembea kwa urahisi katika changarawe. Kwa jumla mumbile ya ngamia humsaidia kuweza kuyahimili mazingira magumu ya jangwani.

Watu wanaomfuga ngamia humtumia katika uchukuzi wa mizigo na hata kuwabeba watu. Kwa hivyo, huwa mwenye manufaa sana kwa watu wanaoishi jangwani. Kwa vile sehemu za jangwani hazina magari ngamia huchukua nafasi hiyo.

Mbali na kuwa ni chombo cha uchukuzi jangwani ngamia huwapatia wanao mfuga maziwa na mnyama. Waarabu na Wasomali huyapenda maziwa ya ngamia sana. Huyatumia kama chakula. Nyama ya ngamia ina mafuta mengi na huwa ni chakula bora kwa wanaomfuga

Maswali.

1. Ngamia hutumiwa na watu wanaoishi?

2. Ngamia anaweza kwenda safari ndefu bila?

3. Taja faida moja ya ngamia?

14. Sehemu ya ngamia iliyoinukia mgongoni inaitwaje? _____
15. Wanaomtumia ngamia ni akina nani?

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Ulegevu ni adui, kwa maisha ya faraja
Mtu haumnyanyui, toka chini juu kuja
Kisha hautuzindui, kufaraji zetu haja
Ulegevu ni adui, nyumba ya umaskini.

Kila aina ya dhiki, I ndani ya ulegevu
Moyo kukosa ashiki, kutenda kitu kwa nguvu
Hukosekana riziki, nyumba ya watu wavivu
Ulegevu ni adui, nyumba ya umaskini.

Hautufai uzembe, wala ni jitimai
Kukaa kutwa tuombe, jambo halituokoi
Jamani tushike jembe, ulegevu haufai
Ulegevu ni adui, nyumba ya umaskini.

Maswali.

1. Shairi hili lina beti ngapi? _____
2. Kila ubeti katika shairi hili una mishororo mingapi? _____
3. Katika ubeti wa pili, mshairi anaeleza kuwa ulegevu una hasara gani? _____
3. Andika kibwagizo cha shairi hili _____
4. Kulingana na shairi, mtu **mzembe** ni mtu wa _____

aina gani? _____

tumia jibu lifaalo kujaza mianya

15. Salamu ya heshima kwa mtu anayekuzidi umri ni _____

16. Viti 906,069 huandikwaje kwa maneno _____

17. Pigia mstari neno ambalo halipatikani katika ngeli ya KI-VI.(Kikombe,kipepeo, kijiti).

18. Taja chombo kimoja cha usafiri. _____

19. Shibli ni kwa simba ilhali _____ ni kwa paka.

20. Makau alitumia tunda jekundu la duara kuungia _____

kitoweo. Tunda hilo ni lipi? _____

21. Kamilisha methali, "Njia ya mwongo ni _____"

22. Aina ya pikipiki lakini ina magurudumu matatu, _____

moja mbele na mawili nyuma ni _____

23. Fumbua fumbo, "Ninataka kukaanga mayai nina viungo vyote ninavyohitaji na vifaa vyote ninavyohitaji. Je, nimekosa nini?" _____

24. Kanusha sentensi hii. "Gari lote limeoshwa." _____

25. Msimu wa mvua nyingi huitwaje? _____

26. Kisui ni kwa chui ilhali shibli ni kwa _____

27. Ulikuwa ni wakati wa kipindi cha Kiswahili Juma alipomwendea mwalimu wake na kumwambia, _____

"Mwalimu nataka kwenda chooni kukojoa". Je, alifaa kuomba ruhusa vipi huku akizingatia msamiati wa adabu? _____

28. Ikosoe sentensi hii, "Ameshoka kubeba choka" _____

29. Kinyume cha anika ni anua. Je, kinyume cha funga ni nini? _____

30. Andika katika wingi, "Alienda kununua embe" _____

31. Tegua kitendawili, "Mzungu kasimama kwa mguu mmoja" _____

32. Taja rangi moja ya upinde wa mvua _____

33. Karuri aliambiwa na mama yake, "Tafadhali ifagie nyumba ____ote." _____

34. _____ Mzee Jomo Kenyatta alisifika sana kwa uongozi wake.

Andika kwa maneno

35. 10001 _____

36. 120210 _____

Kamilisha sentensi ukitumia kiashiria mwafaka

37. Mahali _____ ndipo shambani petu

38. Kiazi _____ ni kitamu

39. Mto _____ umejaa maji.

40. chupa _____ ina dawa

Tumia viashiria radidi

41. Mvuvi yuko _____ baharini.

42. Miti ipandwe _____ shambani.

Tunga sentensi ukitumia istihara hizi chiriku.

43. _____

Simba

44. _____

Kamilisha sentensi kwa istihara mwafaka.

45. kisu hiki ni (jembe, wembe)kukigusa tu kimekukata.

46. Wageni hawa ni (siafu, watu) sijui watalala wapi wote hawa

Tumia viunganifu vifaavyo.

47. chuma _____ kufungia dirisha.

48. uyoga _____ nyasini si mzuri

Kanusha sentensi hizi.

mikate imeoza

49. _____

wembe umepotea.

50. _____

Majibu

1. B
2. C
3. D
4. D
5. B
6. B
7. B
8. A
9. B
10. D
11. Jangwani
12. Ya kuchoka
13. Uchukuzi
14. Nundu
15. Waarabu na Wasomali
16. Tatu
17. Minne
18. Huleta umaskini
19. Ni adui
20. Shikamoo
21. Viti Elfu mia tisa na sita, sitini na tisa
22. Kipepeo
23. Meli, Ndege, Gari
24. Kipusi
25. Nyanya
26. Fupi
27. Tuktuk
28. Mayai
29. Gari lote halijaoshwa
30. Masika
31. Mwalimu nataka kuenda msalani.
32. Amechoka kubebe shoka
33. Fungua
34. Walienda kununua maembe
35. Uyoga
36. Nyekundu, samawati, kijani,
37. Yote
38. Hayati
39. Elfu kumi, na moja
40. Elfu mia moja na ishirini, mia mbili na kumi.
41. Huk huko
42. Humu, humu
43. Juliani ni chiriku
44. Baba yake ni simba
45. Wembe
46. Siafu.
47. Cha
48. Wa
49. Mikate hajjaoza
50. Wembe hujapotea